**Learning by Ear 2010 – Urban exodus**

**Episode 08: "Love Triumphs"**

**Author: Alfred Dogbé**

**Editor: Yann Durand**

**Translator: Anne Thomas**

WAHUSIKA:

Onyesho la 1:

- **NANA** (UMRI WA MIAKA 22, KIONGOZI WA CHAMA CHA VIJANA)
- **HADIA** (UMRI WA MIAKA 45, MAMA YAKE NANA )

Onyesho la 2:

- **KABO** (MKULIMA, MJOMBAKE BEN, UMRI WA MIAKA 57)
- **HADARI** (UMRI WA MIAKA 48, MKUU WA IDARA YA HUDUMA ZA MASHAMBANI)
- **2 CUSTOMERS**

Onyesho la 3:

- **BAKI** (UMRI WA MIAKA 26, MWANAELIMUJAMII, RAFIKI YAO ZEINA NA BEN)
- **ZEINA** (UMRI WA MIAKA 24, MWANAUCHUMI, RAFIKI YAO BAKI NA BEN)

**Intro:**

Karibu kwenye *Learning by Ear* ili upate kipindi kipya cha mfululizo wetu uitwao “Kukabiliana na Wimbi la Mabadiliko” kuhusu uhamiaji mijini. Ben, Baki na Zeina ni vijana watatu walio na shahada za chuo kikuu lakini hawana ajira. Wameamua kuondokana na dhiki za mji na kwenda kuanzisha chama cha ushirika cha ukulima kijijini mwao. Lakini huko pia wanakabiliwa na matatizo kadha wa kadha. Kwa mfano Hadari, mkuu wa idara ya huduma za mashambani, anawatatiza wanapokwenda kutaka awahudumie. Katika kipindi kilichopita ugomvi kati ya huyu Hadari na Baki, uliishia kwa Baki kupelekwa hospitalini.

Katika kipindi hiki cha nane, tutasikia matokeo ambayo hayakutarajiwa kufuatia masaibu yaliyomkumba Baki.

**Scene 1: At Nana's.**

**NANA AND HADIA.**

1. **ATMO: SOUNDS IN THE KITCHEN: A SAUCE BOILING, A LADLE MIXING THE SAUCE, HITTING AGAINST THE SAUCEPAN.**

2. **HADIA** Nana! ... Yuko wapi? Nana?

3. **SFX: STEPS COMING CLOSER.**

4. **NANA** Nipo hapa, ma!

5. **HADIA** Tayari. Vaa vizuri kisha umpelekee chakula hiki.

| | | |
|---|---|---|
| **6.** | **NANA** | Nani? |
| **7.** | **HADIA** | Mgonjwa wetu! Nimpikie nani mwengine? Hivyo ndivyo unavyomdhibiti mwanamume umpendaye - inakubidi ujipendekeze kwake. |
| **7.** | | |
| **8.** | **NANA** | Mbona sikuelewi? |
| **9.** | **HADIA** | Usiwe hivyo nawe. Baki anakutaka! Nawe pia unampenda. Kwa kuwa sasa yuko hospitalini, mpelekee chakula hiki na ukae naye kidogo. |
| **10.** | **NANA** | Ma! Mbona unayaingilia mambo yasiyokuhusu? |
| **11.** | **HADIA** | Mambo gani hayo yasiyonihusu? Sasa umenikasirikia? |
| **12.** | **NANA** | Unavyofikiria sivyo. Mimi na Baki ni marafiki wa kawaida tu! |
| **13.** | **HADIA** | Mnaonekana pamoja kila wakati. Hakuna siri! |
| **14.** | **NANA** | Basi nakujulisha kwamba Baki na Zeina wanapendana. |
| **15.** | **HADIA** | Ndiyo, hata kama wanapendana sasa lakini Baki atamuoa mwanamke atakayefanikiwa kuudhibiti moyo wake! Nakuhakikishia kwamba ataishia kuwa wako hatimaye! |
| **16.** | **NANA** | Ma, simpendi Baki! Na hata kama ningekuwa nampenda siwezi kufanya jambo ambalo litatatiza mshikamano wa kundi letu na chama chetu. |

**17.** **HADIA** Si wewe uliyesema unataka kujiendeleza kibinafsi kwa kujishughulisha na chama hiki?

**18.** **NANA** Ndio, nilisema. Hilo ndilo lengo kuu la mradi wetu!

**19.** **HADIA** Mwanamke wa kusifiwa ni yupi? Ni ambaye hajaolewa na anayefikiria kazi tu? Usiwe mjinga! Nenda ukabadilishe nguo! Vaa hiyo nguo inayokubana, hiyo nyekundu!

**20.** **NANA** Tayari nilimtembelea Baki asubuhi.

**21.** **HADIA** Kwa hivyo?

**22.** **NANA** Kwa hivyo simpelekei chakula hiki.

**23.** **HADIA** Unajua fedha ambazo nimegharamika kwa chakula hiki?

**24.** **NANA** Sikukwambia mimi ninataka chakula hicho.

**25.** **HADIA** Haya basi, nitakipeleka mimi mwenyewe!

**26.** **NANA** Hapana! Hapana! Tafadhali ma! (**sighing**) Sawa. Sawa nitajitayarisha sasa hivi nimpelekee.

**27.** **SFX: STEPS GOING AWAY**

**28.** **HADIA** (**triumphant laugh**) Mnafiki! Hujui hata mimi niliwahi kuwa na umri wa miaka ishirini? Hawakuniita “mpatanishi” bure wala siwezi kukubali binti yangu azeekee nyumbani. Vipi nikajaaliwa kupata binti mwenye haya hivi? Mwenyewe ana haya tele ilhali ana kila lenye kuwavutia wanaume!

**29.** **SFX: (RAPID STEPS APPROACHING)**

**30. HADIA** Unapendeza si haba! Ukifika kwake tafadhali utabasamu kidogo nawe…!

**31. SFX: (STEPS GOING AWAY)**

**32. HADIA** ....Yaachie mapenzi yakuongoze mwanangu!

**33. SFX:(SOUND OF A GATE SHUTTING VIOLENTLY )**

**34. HADIA** Na baada ya yote hayo anajifanya ati amekasirika! (**laughter**)

**----- MUSIC -----**

**Scene 2: Bar.**

**HADARI, KABO, TWO CUSTOMERS.**

**35. SFX: LOUD BAR ATMOSPHERE: SHOUTS, CONSERVATIONS, DANCE MUSIC**

**36. CLIENT 1** Huyo bwana mzuri! Amekuwa akicheza muziki bila kusita kwa muda wa saa. Na yuko sawa. Mitindo yote anaijulia.

**37. CLIENT 2** Anaitwa Hadari, ni mkuu wa idara ya huduma za maendeleo ya mashambani. Amezoea kuja hapa.

**38. CLIENT 1** Kwani anasherehekea?

**39. CLIENT 2** Nadhani hivyo… Lakini hata kama ni kusherehekea mtu hanywi pombe vile, tena peke yake.

**40. ATMO : HANDS CLAPPING MORE AND MORE RYTHMICALLY**

**41. CLIENT 1** Ebu mwangalie! Tazama! Huyo bwana ni moto wa kuotea mbali, bila shaka!

**42. ATMO: LOUD CLAPS AND CRIES OF ENCOURAGEMENT**

**43. SFX: THE MUSIC CHANGES**

**44. HADARI** (**drunk and out of breath**) Kuna nini? Ebu pigeni muziki halisi! Hujambo Bwana Kabo! Umekuwa hapa tangu lini? Samahani sijakuona. Nilikuwa nikicheza muziki. Karibu ukae kwenye meza yangu. Njoo!

**45. SFX: NOISE OF CHAIRS BEING MOVED**

**46. KABO** Ulitaka kuzungumza nami?

**47. HADARI** Ndiyo! Si jambo kubwa! Karibu kinywaji! Tuna muda wa kutosha. Tena tuko hai, au siyo?

**48. KABO** Afadhali tuahirishe kikao hiki. Pengine tukutane kesho.

**49. HADARI** Hapana, hapana. Ni jambo muhimu na tena ni la dharura! Pokea!

**50. KABO** Nini hiki?

**51. HADARI** Chama chenu kimepata kibali. Tazama hapo chini. Sahihi ya mkuu wa eneo. Unaiona? Iko sawa, au siyo? Nilitaka nikupe wewe binafsi.

**52. KABO** Sijui nikushukuru vipi. Sikutarajia…

**53.** **HADARI** Acha hiyo! Mimi ndiyo napaswa nikushukuru. Nimehamishiwa eneo jingine.

**54.** **KABO** Umehamishiwa eneo jingine?

**55.** **HADARI** Ndiyo, lakini nina mwezi mmoja. Na kwa kweli wala si adhabu. Hapa nilikuwa nimeshaanza kuvurugikiwa. Huko niendako ni afadhali. Wakati haya yote yalipotokea hakuna hata mmoja aliyetaka kuniona. Ushahidi wako ilinisaidia sana.

(**voice chokes up**)

... nimekuwa hapa kijijini kwa … miaka 10…na sijawahi kumuudhi mtu yeyote. Lakini hata hivyo walitaka kuniua. Walipeleka barua kwenye ofisi kuu ya eneo wakitaka nihamishiwe mahali pengine. Lakini kwa bahati ulikuwa shahidi pekee. Asante sana. Ninakushukuru sana!

**56.** **KABO** Mimi… eeh… nina…ee..ni …

**57.** **HADARI** Usiseme lolote. Ndiyo hali ya maisha. Ndivyo watu walivyo. Na unajua, chama chenu ndiyo tegemeo la baadaye. Nitakudokeza jinsi mnavyoweza kusaidiwa kifedha.

**58.** **KABO** Alaa, kweli?

**59.** **HADARI** Naam, msaada kwa miradi mipya mizuri kama huo wenu. Mtapata fedha nyingi, tena kwa njia ya halali, nakuhakikishia.

**60.** **KABO** Niende kwa nani?

**61. HADARI** Njoo kwangu. Nitakupatia habari yote.

**62. KABO** Tungependa kujua habari hiyo!

**63. HADARI** Siyo tu ya kuvutia, lakini bahati kubwa hiyo. Mnatakiwa kujaza fomu chache haraka iwezekanavyo. Vijana wako ni wachapakazi na wenye vipaji. Tena wanaaminika!

**64. KABO** Iweje hawaijui habari hii? Ben alikuwa na nyadhifa muhimu wizarani. Mbona hajui jambo hili?

**65. HADARI** Hujui binadamu walivyo – watakuficha habari ili wajifaidi wao tu. Lakini mara nyingi hawatimizi masharti yaliyowekwa.

**66. KABO** Hatimaye hakuna anayefaidika.

**67. HADARI** Ndiyo hivyo! Fedha hizo hupotea vivi hivi!

**68. KABO** Jambo la kusikitisha!

**69. HADARI** Bila shaka. Unafahamu kuwa kijiji chetu hakipati hata robo ya fedha kilizotengewa? Kwa muda wa miaka mitatu nimekuwa nikinuia kupeleka maombi ya fedha hizo. Lakini kila mwaka huchelewa. Na ukichelewa, matokeo yake ndiyo hayo…

**70. KABO** Nitakuja ofisini kwako kesho.

**71. HADARI** Vyema. Najisikia mchovu sana. Lakini yote niliyokuambia ni mambo ya kweli! Ukweli mtupu! Ninakuhakikishia hilo! **(MORE DANCE MUSIC SOUNDS)** Hatimaye muziki halisi… Samahani, ninataka kucheza muziki… Tutaonana kesho

ofisini kwangu!

**----- MUSIC -----**

**Scene 3: Clinic.**

**BAKI AND ZEINA.**

**72. ATMO: CLINIC SOUNDS. OBJECTS BEING PUT AWAY (SCISSORS, SYRINGE, MEDICINE). TROLLEY GOING BY.**

**73. ZEINA** Muombe daktari upelekwe mjini ukachunguzwe zaidi.

**74. BAKI** Una wasiwasi wa nini? Daktari mwenyewe anashangaa ninavyoendelea kupata nafuu. Hali yangu si mbaya sana.

**75. ZEINA** Usiyachukulie mambo hivi hivi – si ajabu ukapata matatizo...

**76. BAKI** Matatizo gani? Ninapata maumivu ya kichwa mara kwa mara lakini yataisha. Hali yangu nafuu sasa. Vipi chama chetu?

**77. ZEINA** Tumeshapata idhini!

**78. BAKI** Jambo zuri sana hilo!

**79. ZEINA** Hapa nina jingine zuri zaidi. Umejishindia kibali cha kuhamia Marekani!

**80. BAKI** Je, kweli wanakijiji walitaka kumwangamiza Hadari?

**81. ZEINA** Alikimbizwa kupitia kijijini. Kama si Kabo na wazee wengine kuingilia kati, angekipata. Hata alivukwa na kiatu chake ambacho kilichukuliwa na baadhi ya watoto waliokuwepo...

**82.** **BAKI** (**laughter … then a cry of pain**) Aaah!

**83.** **ZEINA** Una nini?

**84.** **BAKI** Kichwa changu…Sipaswi kucheka.

**85.** **ZEINA** Bora uende mjini kwenye hospitali halisi na pia uende ukashughulikie mambo yako. Una siku tano tu za kuishughulikia viza yako.

**86.** **BAKI** Zeina…! Siendi. Hayo sasa yamepita. Ninawashukuru ninyi nyote. Niambie kuhusu Hadari na wanakijiji… Nataka kujua yaliyonipita huko kijijini.

**87.** **ZEINA** Kutokana na juhudi za Hadari chama chetu sasa kitapata ufadhili wa kitita kikubwa cha fedha.

**88.** **BAKI** Hadari...? Kweli? Binadamu wana maajabu yao.

**89.** **ZEINA** Baki, nimekuwa nikiliwazia hili jambo letu mimi nawe. Nasikitika sasa kwamba nimekuvutia kujiingiza kwenye balaa yote hii.

**90.** **BAKI** Bila wewe, nisingekuwa hapa. Ninakushukuru sana. Waona mambo tuyafanyayo katika kijiji hiki? Mabadiliko tunayoleta?

**91.** **ZEINA** Tafadhali Baki, nisikize!

| | | |
|---|---|---|
| **92.** | **BAKI** | Unataka nini? Sikuwa na nia ya kuja hapa. Nilidhani hatungeweza kufanya lolote humu nchini lakini wewe ukanishinikiza. Ulinilazimisha kufuata ulivyotaka. Sikuwa na ujanja. Nilikuja huku kwasababu ninakupenda. Sikutaka kukupoteza. Nilidhani kwamba maisha ya huku yangekumakinisha. Sasa hivi mafanikio ya kazi yetu yako njiani, mbona unanitaka niondoke? |
| **93.** | **ZEINA** | Ndiyo! Sitaki uteseke kwasababu yangu mimi! Ukishafika huko na kumakinika, nitaungana nawe! Tafadhali Baki, yazingatie maneno yangu! |
| **94.** | **BAKI** | Haiwezekani! Kama unanipenda kweli, nisaidie nitayarishe mustakabali wangu hapa. Mustakabali wetu! |
| **95.** | **ZEINA** | Huambiliki husemezeki! |
| **96.** | **BAKI** | Dalili tosha kwamba bado nakupenda – msichana asiyetabirika! |
| **97.** | **ZEINA** | Natumai utaendelea kunipenda na hapo utagundua kwamba ninatabirika. |
| **98.** | **BAKI** | Swali hilo ama ni dua? |
| **99.** | **ZEINA** | Ni swali na ni dua! Ndiyo au hapana? |
| **100.** | **BAKI** | Hapana! |
| **101.** | **ZEINA** | Mwongo! |

**102. ZEINA & BAKI** (**laughing… Then kissing**)

**Outro:**

Hivi ndivyo kipindi cha leo cha *Learning by Ear* kinavyokamilika.

Ni mfululizo wa vipindi kuhusu uhamiaji mijini.

Tunakushukuru kwa kutusikiliza. Usikose kipindi kitakachofuata ili ujue iwapo chama cha ushirika kimefanikiwa kukabiliana na changamoto zinazokikumba.

Ikiwa unataka kukisikiliza tena kipindi hiki au kutupatia maoni fungua ukurasa wetu wa tovuti dw-world.de/LBE au utuandikie barua-pepe kupitia anwani yetu lbe@dw-world.de.

Usisahau kututegea sikio kwenye kipindi kijacho!

**END OF EPISODE 8**